# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

# TAARIFA FUPI YA FURSA ZA UWEKEZAJI ZINAZOPATIKANA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA

# SIKONGE

## i. DIBAJI

Maendeleo ya Sikonge yanategemea upatikanaji wa fursa za uwekezaji. Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 sambamba na MKUKUTA awamu ya pili (NSGRP II) na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) unatarajiwa kutumia ipasavyo fursa zilizopo katika Mkoa wa Tabora.

Wasifu huu umeandaliwa ili kusaidia katika kutathmini fursa za uwekezaji zilizopo kwa lengo la kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na wa nje kuchangia kufanikisha ndoto ya kujenga wilaya.

Mbali na fursa za uwekezaji zilizobainishwa kwenye wasifu huu, zipo sababu nyingine nyingi zinazopaswa kumvutia mwekezaji kuja Sikonge. Sababu hizo ni pamoja na hali nzuri ya hewa, wilaya ina hali ya amani na utulivu wa kisiasa, upatikanaji wa nguvu kazi, miundombinu ya usafiri na rasilimali nyingi za asili.

Sikonge imeweka kipaumbele katika baadhi ya fursa za uwekezaji Fursa hizo ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji (hasa kilimo cha mpunga), ufugaji wa ng'ombe wa kunenepesha, ufugaji wa samaki katika mito na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi.

Kwa niaba ya wananchi wa wilaya ya Sikonge, ninapenda kuwakaribisha wawekezaji wote wenye nia njema kuelekeza mitaji yao katika wilaya ya Sikonge ili kufaidika na fursa lukuki zilizopo

## 1.0 Utangulizi

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilianzishwa mwaka 1995 ni kati ya Halmashauri zinazounda Mkoa wa Tabora na inapatikana Kusini mwa Mkoa wa Tabora, Kilomita 76 kutoka Manispaa ya Tabora. Wilaya ya Sikonge inapakana na Wilaya ya Urambo upande wa Kusini Magharibi, Wilaya ya Manyoni upande wa Mashariki, Wilaya ya Uyui upande wa Kaskazini na Wilaya ya Chunya upande wa Kusini.


### 1.1.Eneo na Idadi ya Watu

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ina eneo lenye Kilomita za Mraba ($Km^2$) **27,873,** sawa na asilimia **27** ya eneo lote la Mkoa wa Tabora, ambapo **94.5%** ya eneo hili ni hifadhi ya misitu na **5.5%** ni eneo la makazi na shughuli za uzalishaji. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 Wilaya ina watu **335,686**, kati ya hao wanaume ni **165,309** na wanawake ni **170,377**. Wilaya hupata mvua kwa wastani wa **800mm** hadi **1300mm** kwa mwaka. Hata hivyo kiwango cha mvua kwa mwaka kimeshuka na kufikia **600mm** hii ni kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yanahusishwa na uharibifu wa mazingira.

### 1.2.Utawala

Halmashauri ya Wilaya ina Tarafa **2** ambazo ni Sikonge na Kiwere, Kata zipo **20**, Vijiji **71** na Vitongoji **286**. Wilaya ina Jimbo **1** la Uchaguzi. Aidha kuna madiwani **27** ambapo madiwani **20** ni wa kuchaguliwa na **7** ni madiwani viti maalum.

# RAMANI YA HALMSHAURI YA WILAYA YA SIKONGE



**1.3.Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Wilaya.**

Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge wanategemea zaidi shughuli za Kilimo na Ufugaji, ambapo Sekta ya Kilimo imeajiri zaidi ya **80%** ya wakazi wa Sikonge. Shughuli nyingine ni ufugaji wa Nyuki, Biashara, Uvuvi, Uchanaji mbao, Ajira rasmi katika taasisi mbalimbali na uchimbaji madini.

## 2.0 FURSA ZA UWEKEZAJI ZINAZOPATIKANA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YASIKONGE.

### 2.1 Maeneo ya Biashara na uwekezaji katika kilimo.

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ina eneo la Hekta **2,787,300** hata hivyo takribani **94.5%** ni eneo la misitu, eneo linalobaki **5.5%** ndiyo eneo la makazi na shughuli za kiuchumi, ambapo eneo linalofaa kwa kilimo ni Hekta **140,465** sawa na **5%** na eneo linalolimwa ni Hekta **84,678** sawa na asilimia **ya 60 eneo lote linalofaa kwa kilkimo.** Mazao ya biashara yanayolimwa ni tumbaku, karanga, korosho na alizeti. Kwa upande wa chakula mazao yanayolimwa ni mahindi, mpunga, maharage, viazi vitamu na mihogo.

Wilaya ina makampuni **(10)** yanayojishughulisha na ununuzi wa Tumbaku, makampuni hayo ni **MKWAWA LEAF TABACO, ALLIANCE ONE, JTILS, MAGEFA, G-4 AGRO, BIEXEN, GLTL, MILAMBO, FEMOUS ROCK, OBAMCO NA 3H** .

**2.1.2** Uzalishaji wa mazao kama karanga (tani10,393 )na alizeti (tani3,484) unatoa fursa ya ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao haya.

**2.1.3** Upatikanaji wa matunda aina ya maembe (tani **18,720**), matikiti maji (tani **2,223**) na mapapai (tani **288**) unatoa fursa ya kujenga viwanda vya kusindika matunda haya. Kwa sasa matunda haya hutumika/husafirishwa nje ya wilaya bila kuongezwa thamani.

**2.1.4** Pia kuna fursa ya kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya nafaka. hivi sasa uzalishaji wa mahindi (tani **34,657,000**) na mpunga (tani **25,776,000**) ili kuongeza thamani ya mazao haya. Hivyo basi tunapenda kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya mkoa wa Tabora kutumia

fursa hizi za ujenzi wa viwanda hasa ikizingatiwa Halmashauri imeshatenga eneo la ujenzi wa viwanda vikubwa na vidogo.




*Mahindi yakiwa shambani*



*Mahindi yaliyokauka*



*Zao la Mihogo*

*Zao la mpunga* *Zao la viazi vitamu*



*Zao la karanga linatumika kama chakula na kama za la biashara*




*Zao la tumbaku kwa ajili ya biashara*



*Mti wa embe ndogo ndogo (Embe sindano)*

### 2.1.1 Kilimo cha Umwagiliaji

Wilaya ya Sikonge ina jumla ya Hekta **1,550** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ambapo eneo lenye Miundombinu ya umwagiliaji ni Hekta **375** na eneo linalolimwa ni Hekta **214**. Mazao yanayolimwa kwa umwagiliaji ni mpunga, mahindi na mbogamboga . Wilaya ina Skimu **(3)** za umwagiliaji ambazo ni Ulyanyama.(Kata ya Kisanga na Igigwa), Igigwa ( Kata ya Igigwa) na Uluwamibono(Kata ya Kiloleli). Ambapo uzalishaji katika skimu hizi kwa sasa ni tani **1070.** Wafanyabiashara wenye mitaji wanakaribishwa kuja kuwekeza kwa kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa Skimu na Miundombinu ya umwagiliaji, pamoja na kushiriki katika kilimo cha umwagiliaji na kujenga viwanda vya kuchakata mchele kwenye kata/vijiji vilivyo na skimu za umwagiliaji.

*Skimu ya Umwagiliaji Uluwa*

## 2.2 Fursa za biashara zitokanazo na sekta ya mifugo.

Halmashauri ya Wilaya ina jumla ya mifugo **1,046,190** wakiwemo ng'ombe **353,502**, mbuzi **123,661**, kondoo **19,081**, nguruwe **3,290**, mbwa **15,687** paka **3,762**, kuku **515,493**, bata **11,101** na punda **613.** Aidha, wapo wataalamu wanaotoa huduma za ugani kwa wafugaji.

2.2.1 Fursa zinazopatikana kutokana na mifugo ni kufungua viwanda vya kusindika ngozi na pembe za ng'ombe ambazo kwa sasa havipo, kufungua vituo vya kunenepesha mifugo, kutoa ushauri na kutibu mifugo, maduka ya madawa ya mifugo.

2.2.2 Kujenga viwanda vya kusindika mazao ya mifugo kama nyama na maziwa, ambapo kwa sasa mifugo husafirishwa nje ya Wilaya bila kuongezewa thamani.

2.2.3 Kujenga vituo vya kufuga kuku wa kienyeji na kukusanyia mayai ya kuku wa kienyeji. Hii ni kutoka na Wilaya kuwa na uzalishaji wa mahindi na mpunga hivyo upatikanaji wa chakula cha mifugo ni wa huhakika.

2.2.4 Pia kuna fursa ya kutengeneza miundo mbinu katika sekta ya mifugo, ambayo ni majosho, mawe ya kuchinjia, machinjio, clinic za mifugo na maabara za mifugo. Ambapo kwa sasa Halmashauri ina machinjio 1 na mawe ya kuchinjia 3.





Kuku wa kienyeji Ng'ombe wakiwa machungani

## 2.3 Madini

Mwaka 2013 madini aina ya dhahabu yaligundulika katika kijiji cha Kapumpa , Kata ya Kitunda ambako uchimbaji wa madini hayo unafanywa na wachimbaji wadogo wadogo wa ndani na nje ya Wilaya pamoja na makampuni ya machimbaji wadogo. Uchimbaji huu unafanyika katika eneo la wazi na wachimbaji wengi wadogo wadogo wanatumia teknolijia duni katika kuchimba na kusafisha dhahabu. **Hivyo fursa ipo kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika uchimbaji wa madini kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji.**





*Mashimo ya kutoa dhaabu katika Mgodi wa Kitunda*





*Mchanga uliochimbwa tayari kusafishwa katika mgodi wa Kitunda.*

## 2.4 Maeneo ya uwekezaji wa kibiashara (Vituo vya mafuta, mahoteli, mabenki n.k).

Katika Wilaya ya Sikonge kuna benki **3** ambazo ni NMB, CRDB na TCB zinazotoa huduma za kifedha kwa wananchi wa kata ya Sikonge. Pia kuna Taasisi 18 ndogondogo za fedha zinazo wahudumia wananchi waishio Sikonge.

Kata 4 hazina huduma za vituo vya mafuta,Vilevile ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Tabora mpaka Mpanda Mkoani Katavi na baadaye kutoka Ipole mpaka Mbeya kunatoa fursa kwa wawekezaji kuwekeza katika ujenzi wa vituo vya mafuta, kwa ni kwa sasa Wilaya ina vituo 4 vya mafuta ambapo vituo hivi vinapaitikana kata za Tutuo 1, Kata ya Sikonge 2 na Kata ya Ipole 1. Kata 4 hazina huduma za vituo vya mafuta ambazo ni kitunda km 180 kutoka Sikonge, kiloli, kilumbi na kipili.

2.4.1 kutokana na uboreshaji wa miundo mbinu ya barabara, kuna uhitaji wa ujenzi wa hotel na nyumba za kulala wageni kwani magari ya abiria na mizigo yanayo kwenda Mpanda na Mbeya kupitia Sikonge yameongezeka sambamba na kuongezeka kwa wasafiri. Hivyo wawekezaji wanaombwa kutumia fursa hii kwa maendeleo yao binafsi na wilaya kwa ujumla.






*Benki ya Biashara ya NMB* *Benki ya Biashara ya CRDB*

## 2.5 Maeneo ya uwekezaji wa viwanda.

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imeendelea kutekeleza juhudi za Serikali ya kujenga nchi yenye uchumi wa viwanda. Ili kutekeleleza azma hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imetenga eneo lenye jumla ya hekta **1,390.63** kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa na vidogo. Eneo hilo lipo katika kata ya Sikonge ambapo kati ya hekta hizo **1,390.63,** hekta **416.66** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogovidogo na hekta **973.97** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa. Tunawakaribisha wawekezaji kuwekeza katika viwanda vidogovidogo na vikubwa na vya kati kwa kuzingatia malighafi zinazopatikana ndani ya Wilaya ya sikonge kama vile mazao ya kilimo, mbao na asali .( aina ya viwanda)

## 2.6 Fursa za biashara zinazotokana na Misitu

Sikonge ina jumla ya misitu ya hifadhi 9 ambapo misitu **4** ni ya Serikali Kuu na misitu **5** ni ya Halmashauri. Misitu hii yote kwa ujumla ina eneo la **hekta 1,992,456** kama inavyooneshwa hapo chini, misitu ya Hlamashauri ina ukubwa wa **hekta 517,760**

| **Na** | **Jina la msitu** | **Mmiliki** | **Ukubwa Eneo(Ha)** |
|---|---|---|---|
| 1 | Nyahua Mbuga | Serikali kuu | 679,896 |
| 2 | Itulu Hill | Serikali kuu | 384,000 |
| 3 | Iswangala | Serikali kuu | 268,800 |
| 4 | Inyonga East | Serikali kuu | 142,000 |
| 5 | Ugunda | Halmashauri | 128,000 |
| 6 | Ipembampazi | Halmashauri | 133,120 |
| 7 | Walla | Halmashauri | 158,720 |
| 8 | Goweko | Halmashauri | 41,600 |
| 9 | Sikonge | Halmashauri | 56,320 |
| | **Jumla Kuu** | | **1,992,456** |

### 2.6.1 Ufugaji Nyuki

Ufugaji nyuki ni mojawapo ya shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika Wilaya ya Sikonge. Wilaya ya Sikonge inajumla ya wafugaji nyuki **6,555**, na kwa mwaka inazalisha wastani wa tani **2,000** za asali, wakati Wilaya ina uwezo wakuzalisha takribani tani **6,000**. Uzalishaji uko chini kutokana na matumizi ya teknolojia duni inayotumika katika ufugaji nyuki kwani Mizinga ya kienyeji (**367,440**)(Traditional Beehives) ndio inayotumika zaidi kuliko mizinga ya kisasa (**24,228**) (Modern Beehives). Hivyo basi utumiaji wa teknolojia duni unapelekea uzalishaji wa asali kuwa mdogo na wa kienyeji (Local Small Scale Production) na kushindwa kuzitumia rasilimali za mapori kwa kiwango kinachotakiwa (Full utilization of forest resources).



*Mizinga ya kisasa ikiwa imetundikwa katika miti ya miombo katika mapori ya misitu ya Iswangalla*

#### 2.6.1.1 Fursa za biashara na uwekezaji katika ufugaji nyuki

1. Kusambaza teknolojia kwa kutengeneza na kuuza vifaa vya kisasa vya kufugia nyuki kama vile mizinga ya kisasa, mavazi ya kisasa yanayovaliwa wakati wa kuvuna asali. Kwani wafugaji nyuki wengi wanatumia mizinga ya magome ya miti ambayo ina tija ndogo kwani ina uwezo wa kubeba Kg **14** tu za asali, vilevile mizinga hii siyo rafiki kwa mazingira. Mizinga ya kisasa kwa upande wake, ina ujazo mkubwa kwani inaweza kutunza hadi **Kg 40** kwa kila mzinga na vilevile ni rafiki wa mazingira. Aidha, wafugaji wengi wa nyuki wanatumia moto kufukuza nyuki wakati wa kuvuna asali, njia hii inasababisha baadhi ya nyuki na wadudu wengine kufa sambamba na kuchoma misitu inayopelekea uharibifu mkubwa wa misitu na malisho ya wanyama pori. Matumizi ya mavazi maalum na vifaa vya kisasa vya kuvunia asali kutapelekea asali kuwa safi, bora na kuzuia uharibifu wa mazingira sambamba na kutokuua viumbe hai. Hivyo basi wafanyabiashara wenye mitaji wanakarabishwa kuja kuwekeza katika kutengeneza mizinga ya kisasa na kuuza kwa wafuga nyuki sambamba na kuuza mavazi maalum na vifaa vya kisasa vya kuvunia asali.



*Mizinga ya kisasa ikiwa katika eneo la kufugia nyuki*

2. Kununua asali inayozalishwa na kusafirisha kwenda kuuza ndani na nje ya Tanzania kwani mahitaji ya asali na nta katika soko la dunia yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Hii inatokana na watu kujua faida za matumizi ya asali kwa afya ya binadamu kwani asali imekuwa ikitibu maradhi mbalimbali.

3. Taasisi za kifedha zinahamasishwa kutoa mikopo kwa wafugaji nyuki. Taasisi za kifedha zina fursa ya kutoa mikopo kwa vyama vya ushirika vya wafuga nyuki na mfuga nyuki mmoja mmoja ili kuwawezesha kununua vifaa vya kisasa vya kufugia nyuki na kuvunia asali. Mabenki yote ya biashara kama vile Benki ya **NMB, CRDB, NBC, Posta Benki, ABC, Exim Bank** n.k na Taasisi ndogondogo za fedha (Micro finance Institutions) kutoa mikopo kwa gharama nafuu kwa wafugaji nyuki.




*Bango linaloonesha kimojawapo ya Chama cha Ushirika cha Wafuga Nyuki cha IGUNAVAPINA kinachopatikana Wilayani Sikonge*

**4. Fursa ya soko la asali na nta.**

Kwa sasa Halmashauri ina kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki. Ujenzi wa kiwanda hiki unasaidia uzalishaji wa asali kwani walinaji wa asali wanakuwa na uhakika wa kupata soko.

### 2.6.2 Uvunaji wa magogo na Uchanaji wa mbao

Uvunaji wa magogo na Uchanaji wa mbao ni shughuli zinayofanyika katika misitu na mapori yaliyopo Wilayani sikonge. Mbao zinazozalishwa kwa wingi wilayani Sikonge ni mbao za Mninga, mkola, Mkulungu na mtundu. Uvunaji unaruhusiwa kwenye msitu wa Ipembampazi wenye ukubwa hecta 133,120 ambao umefanyiwa mpango wa uvunaji



*Mbao zilizochanwa*

Fursa zinazopatikana na uvunaji wa magogo na uchanaji wa mbao


1. Kujenga viwanda vya kutengeneza samani kama vile viti, meza na makabati ya Ofisini na majumbani, makochi, milango na madirisha.
2. Biashara ya kuuza magogo na mbao ndani na nje ya Wilaya.

### 2.7 Fursa za biashara zinazopatikana katika eneo la Utalii

Wilaya ya Sikonge inafahamika kwa vivutio vya utalii katika mkoa wa Tabora. Kuna mbuga kama vile Ipembampazi, Iswangala, Ugunda na Itulu ambazo zina aina mbalimbali ya wanyama na ndege kama vile Simba, Tembo, Twiga, Nyati, Pundamilia, Mbwa mwitu, Nyumbu, Mbuni, Fisi, swala, Chui, mwewe, kanga na wengine wengi.

Fursa za kibiashara zinazopatikana kutokana na utalii ni zifuatazo:-

(a) Ujenzi wa hoteli za kitalii
(b) Kuanzisha makampuni ya kuwaongoza watalii (Tour guides groups/company)
(c) Kampuni za kusafirisha watalii kwa magari maalum ya utalii.

*Picha ya Twiga na Simba katika mbuga ya Ipembampazi*

### 2.8 Fursa za uwekezaji kwenye mitandao ya Simu

Katika Wilaya ya Sikonge kuna mitandao ya makampuni 4 ya Simu ya Airtel, Vodacom, Yas na Halotel. Makampuni haya yanatoa huduma ya mawasilianona miamala ya kifedha kwa wananchi waishio vijiji tofauti tofauti wilayani Sikonge. Kuna baadhi ya vijiji havijaunganishwa na mitandao ya simu kabisa au kuna kampuni moja tu. Hivyo basi fursa ya kuweka minara mingine inapatikana katika baadhi ya maeneo ambayo hayana mitandao ya simu.

### 2.9 Fursa za uwekezaji kwenye sekta ya elimu.

#### 2.9.1 Secta ya elimu ya msingi

Wilaya ya sikonge kwa mwaka wa masomo **2025** ina shule za msingi zipatazo **112**, kati ya shule hizi, shule **109** ni za serikali na shule **3** za binafsi. Wilaya ina wanafunzi **64,073** kati ya hawa wavulana ni **30,091** na wasichana ni **33,982.** Wastani wa kiwango cha ufaulu ni asilimia **50.49** kwa (takwimu za mwaka **2024).** Wawekezaji

wanakaribishwa kuwekeza katika secta hii kwani shule binafsi ni chache ikilinganishwa na shule za serikali. (Sera )

**2.9.2 secta ya elimu ya sekondari.**

Wilaya ya sikonge kwa mwaka wa masomo **2025** ina shule za sekondari zipatazo **22**, kati ya shule hizi, shule **22** ni za serikali na shule **2** za binafsi. Wilaya ina wanafunzi **9,108** kati ya hawa wavulana ni **4080** na wasichana ni **5028.** Wastani wa kiwango cha ufaulu ni asilimia **100** kwa kidato cha 6, asilimia 89 kwa kidato cha 4 na asilimia 73.3 kwa kidato cha 2 (takwimu za mwaka **2024).** Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika secta hii kwani shule binafsi ni chache ikilinganishwa na shule za serikali, kwani wazazi hulazimika kupeleka wanafunzi nje ya wilaya ili kupata shule binafsi.

Nawasilisha.

Seleman Pandawe

Mkurugenzi Mtendaji (W)

**SIKONGE**